

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
BODI YA KOROSHO TANZANIA

# JARIDA LA KOROSHO
# KUANZIA DESEMBA 1 - 15, 2022



**VOL. 1 CBT.Na.0004**
**Imeandaliwa na:**
**Bodi ya Korosho Tanzania**

## 1.0 UTANGULIZI

Uzalishaji wa korosho duniani umekua ukiongezeka kila mwaka kutokana na jitihada zinazoendelea katika nchi mbalimbali kufanya upanuzi wa maeneo ya kilimo cha korosho, pamoja na matumizi ya teknolojiakama vile matumizi ya mbegu bora. Aidha, katika bara la Afrika kumekuwa na jitihada za kuongeza ubanguaji wa korosho pamoja na kuongeza uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na korosho.

## 2.0. MWENENDO WA SOKO KATIKA NCHI MBALIMBALI DUNIANI

### 2.1. Mwenendo wa soko Afrika Magharibi

Kwa mujibu wa mwenendo wa masoko katika nchi za India na Vietnam katika wiki za mwanzoni mwa mwezi Disemba, 2022, bei za korosho ghafi kutoka katika nchi za Afrika Magharibi kwa soko la India na Vietnam zimeshuka kidogo ukilinganisha na ilivyokuwa mwishoni mwa mwezi Novemba, 2022. Korosho ghafi zimeuzwa kati ya dola za Kimarekani 1,100 hadi 1,245 kwa tani kwa kuzingatia ubora.

### 2.2. Hali ya Soko la Korosho Nchini India

Uingizaji wa korosho ghafi kwa India kwa mwezi Oktoba-2022 ulifikia tani 84,974 na bei ya wastani ikiwa dola za Kimarekani 1,340 kwa tani. Katika miezi 10 ya kwanza ya 2022, uingizaji wa korosho ghafi kutoka nje umefikia tani 1,291,392 ambayo ni rekodi mpya ndani ya miaka hii mitatu mfululizo ambapo kiwango cha juu ilikua wastani wa tani 875, 000.

Mauzo ya korosho karanga katika soko la India kwa mwezi Oktoba, 2022 yalikuwa tani 3,221 na bei ya wastani ikiwa ni dola za Marekani 7,817 kwa tani. Katika miezi 10 ya kwanza ya mwaka 2022, mauzo ya nje ya korosho karanga kutoka India yamefikia tani 37,651, na bei ya wastani kuwa dola za Kimarekani 7,777 kwa tani. Kwa ujumla usafirishaji wa korosho karanga huenda ukawa chini kwa mwaka mzima wa 2022 ambapo takribani tani 44,500 zitauzwa nje ya nchi. Ingawa mahitaji ya korosho karanga kwa soko la ndani bado ni thabiti.

### 2.2 Hali ya Zao nchini Vietnam

Soko la korosho ghafi limeendelea kuwa imara katika wiki chache zilizopita kwa korosho zenye ubora wa SHOT 50 - 54. Bei ya korosho ghafi iko juu ikilinganishwa na mwenendo wa bei ya korosho karanga iliyopo sokoni.. Katika miezi 11 ya mwaka 2022, kiasi cha korosho karanga (cashew kernel) kilichosafirishwa nje ya nchi ni tani 472,331 kwa wastani wa dola za Marekani 5,959 kwa tani. Katika takwimu zilizofanyiwa maboresho hadi Novemba, 2022, Vietnam imepokea wastani wa tani 1,801,148. za korosho ghafi huku zaidi ya asilimia 73 ya korosho hizo ikiwa imeingizwa kutoka nchi za Cambodia (tani 716,334), Ivory Coast (tani 451,275) na Ghana (tani 144,647).

Soko la korosho karanga bado halina mabadiliko mazuri na wanunuzi hawana haraka ya kununua kwa sasa. Kuna uhaba wa korosho karanga za madaraja ya W180, W210, na W240 katika soko la Vietnam kwa sasa, hivyo wanunuzi waliopo inabidi wasubiri mazao mapya hadi mwishoni mwa mwezi Machi, 2023 wakati wa msimu wa mavuno nchini Vietnam.

**Jedwali Na.1: Bei za korosho ghafi katika nchi ya India na Vietnam kwa Desemba,2022**

| MWENENDO WA BEI ZA WASTANI ZA KOROSHO GHAFI (RCN) DUNIANI-CASE STUDY YA INDIA NA VIETNAM KWA KIPINDI CHA SEPTEMBA HADI DESEMBA, 2022 | | |
|---|---|---|
| TAREHE | BEI -CIF USD/TON | |
| | BEI YA CHINI | BEI YA JUU |
| Septemba, 2022 | 1,080 | 1,390 |
| 02 Oktoba, 2022 | 1,080 | 1,350 |
| 31 Oktoba, 2022 | 1,050 | 1,280 |
| 05 Novemba, 2022 | 1,100 | 1,400 |
| 27 Novemba, 2022 | 1,100 | 1,400 |
| 12 Desemba, 2022 | 1,100 | 1,330 |
| SOT: 48 - 52 | | |




**Chanzo: Cashewnutinformation**

## 3.0 BEI ZA KOROSHO KARANGA KUTOKA NCHI MBALIMBALI

Bei ya korosho karanga katika nchi mbalimbali hutofautiana kwa kuzingatia kiwango cha uzalishaji, gharama za uzalishaji pamoja na teknolojia inayotumika kubangua korosho ghafi.

## 3.1 Bei Ya Korosho Karanga Vietnam Kufikia Wiki ya Kwanza Desemba, 2022

Nchini Vietnam bei ya korosho karanga iko chini ukilinganisha na bei katika nchi zingine zinazobangua korosho. Jedwali Na. 2 linaonesha bei ya korosho karanga hadi kufikia mwanzoni mwa mwezi Disemba, 2022.

**Jedwali Na. 2**

| BEI YA KOROSHO KARANGA VIETNAM HADI KUFIKIA NUSU YA KWANZA DESEMBA, 2022 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | WW180 | 7.82 | 8.15 | 18,048.56 | 18,810.20 |
| White Whole Cashews 210 | WW210 | 7.05 | 7.27 | 16,271.40 | 16,779.16 |
| White Whole Cashews 240 | WW240 | 5.95 | 6.28 | 13,732.60 | 14,494.24 |
| White Whole Cashews 320 | WW320 | 5.51 | 5.95 | 12,717.08 | 13,732.60 |
| Large Pieces | LP | 3.52 | 4.30 | 8,124.16 | 9,924.40 |
| Small Pieces | SP | 2.97 | 3.30 | 6,854.76 | 7,616.40 |

**Chanzo: Cashewinformation**

## 3.2 Bei Ya Korosho Karanga katika nchi za Afrika Hadi Kufikia Wiki ya Kwanza Disemba, 2022

Hadi kufikia mwanzoni mwa mwezi Disemba, 2022 bei ya korosho karanga kwa nchi za Afrika Magharibi ambazo ni Ivory Coast, Ghana, Benin nk. ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 3

**Jedwali Na. 3**

| BEI YA KOROSHO KARANGA AFRIKA MAGHARIBI HADI KUFIKIA NUSU YA KWANZA DESEMBA, 2022 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | W180 | | | | |
| White Whole Cashews 210 | W210 | 7.599 | 7.930 | 17,538.50 | 18,302.44 |
| White Whole Cashews 240 | W240 | 5.947 | 6.278 | 13,725.68 | 14,489.62 |
| White Whole Cashews 320 | W320 | 5.617 | 5.837 | 12,964.04 | 13,471.80 |
| White Whole Cashews 450 | W450 | 5.176 | 5.507 | 11,946.21 | 12,710.16 |
| White Splits | WS | 4.626 | 4.736 | 10,676.81 | 10,930.69 |
| Large Pieces | LP | 3.194 | 3.414 | 7,371.75 | 7,879.51 |
| Small Pieces | SP | 2.643 | 2.863 | 6,100.04 | 6,607.80 |

**Chanzo: Cashewinformation**

## 3.3 Bei Ya Korosho Karanga Tanzania Zinazouzwa Nje Ya Nchi Hadi Kufikia Wiki ya Kwanza Desemba, 2022

Bei ya korosho karanga zinazobanguliwa na wabanguaji wa ndani na kuuzwa nje ya nchi ni kama inavyoonesha katika jedwali Na. 4


**Jedwali Na.4**

| BEI YA KOROSHO KARANGA TANZANIA ZINAZOUZWA NJE HADI KUFIKIA NUSU YA KWANZA DESEMBA, 2022 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | W180 | 8.00 | 8.30 | 19,156.40 | 19,156.40 |
| White Whole Cashews 240 | W240 | 7.20 | 7.50 | 16,617.60 | 17,310.00 |
| White Whole Cashews 320 | W320 | 6.80 | 7.10 | 15,694.40 | 16,386.80 |
| White Splits | WS | 4.50 | 5.10 | 10,386.00 | 11,770.80 |
| Large White Pieces | LWP | 3.50 | 4.20 | 8,078.00 | 9,693.60 |

**Chanzo: TACP**

Jedwali Namba 5: Uwiano Wa Bei Daraja WW320

| UWIANO WA BEI DARAJA LA WW320 FOB | | |
|---|---|---|
| Nchi | Bei Dola/Kilo | Bei Tzs/Kilo |
| Vietnam | 5.95 | 13,732.60 |
| Afrika Magharibi | 5.84 | 13,471.80 |
| Tanzania | 7.10 | 16,386.80 |



## 4.0 MWENENDO WA ZAO LA KOROSHO NCHINI TANZANIA

Hadi kufikia tarehe 16 Disemba, 2022 wastani wa tani 147,977,299 tayari zimekusanywa na kuuzwa katika ghala za minada kwa thamani ya shilingi 278,126,995,803. Minada ya mauzo ya korosho bado inaendelea katika maeneo mbalimbali nchini, huku bei ya chini ikiwa imeshuka kwa asilimia 0.6 kutoka wiki iliyoishia tarehe 05 Disemba ambapo bei ya chini ilikuwa 1,710 kwa kilo. Bei ya juu bado haina mabadiliko makubwa ambapo imeshuka kwa asilimia 2 katika wiki iliyoishia tarehe 05 Disemba,2022 ambapo bei ya juu ilikuwa Tshs. 1995 kwa kilo. Aidha, ununuzi wa korosho ghafi kupitia soko la awali kwa ajili ya wabanguaji wa ndani bado unaendelea.

Mahitaji makubwa ya korosho ghafi katika nchi wanunuzi yameendelea kuwa katika ubora wa kuanzia SHOT 50 hadi 54 huku uzalishaji hapa nchini ukiwa na madaraja mawili ambayo ni daraja la kwanza (SHOT 44 hadi 47) na daraja la pili (SHOT 48 hadi 54). Hali hiyo imesababisha kuporomoka kwa bei za korosho daraja la pili. Aidha, katika makusanyo yanayoendelea kwa sasa, kiasi cha korosho daraja la pili kimeanza kuongezeka katika baadhi ya maeneo nchini. Hali hii inachangiwa na uwepo wa mvua zilizoanza kunyesha katika maeneo mbalimbali. Wakulima wanaendelea kuhamasishwa kukausha korosho zao kufikia kiwango cha unyevu kisichozidi asilimia 10 ili kukidhi mahitaji ya soko kwa sasa.

Jedwali Na. 7a Muhtasari Bei za Mnada wa Kitaifa Korosho Ghafi

| Muhtasari Bei za Mnada wa Kitaifa Korosho Ghafi | | | |
|---|---|---|---|
| Wiki iliyopita (Novemba 29 hadi Desemba 05) | | Wiki ya Sasa (Desemba 07 hadi Desemba 15) | |
| Mwenendo wa Bei | Wiki | Daraja la Kawaida | |
| | | Bei ya Juu | Bei ya Chini |
| | *Bei ya sasa* | 1,955 | 1,700 |
| | *Bei ya Mnada Uliopita* | 1,995 | 1,710 |
| | *Mabadiliko (%)* | ▼2.0% | ▼0.6% |



**Jedwali Na. 7b Bei ya Mauzo ya Mkoa Korosho Ghafi**

| Bei ya Mauzo Korosho Ghafi ya Mkoa (Desemba 07 hadi Desemba 15) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| MKOA | CHAMA KIKUU | WIKI | Daraja la Kawaida | |
| | | | Bei ya Juu | Bei ya Chini |
| MTWARA | MAMCU | *Bei ya sasa* | 1,945 | 1,700 |
| | | *Bei ya Mnada Uliopita* | 2,000 | 1,800 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | ▼2.8% | ▼5.6% |
| | TANECU | *Bei ya sasa* | 1,955 | 1,939 |
| | | *Bei ya Mnada Uliopita* | 1,990 | 1,930 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | ▼1.8% | ▲0.5% |
| LINDI | RUNALI | *Bei ya sasa* | 1,945 | 1,850 |
| | | *Bei ya Mnada Uliopita* | 1,985 | 1,930 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | ▼2.0% | ▼4.1% |
| | LINDI MWAMBAO | *Bei ya sasa* | 1,726 | 1,726 |
| | | *Bei ya Mnada Uliopita* | 1,725 | 1,720 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | ▲0.1% | ▲0.3% |
| PWANI | CORECU | *Bei ya sasa* | 1,707 | 1,650 |
| | | *Bei ya Mnada Uliopita* | 1,716 | 1,707 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | ▼0.5% | ▼3.3% |
| RUVUMA | TAMCU | *Bei ya sasa* | 1,746 | 1,745 |
| | | *Bei ya Mnada Uliopita* | 1,760 | 1,707 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | ▼0.8% | ▲2.2% |
| MOROGORO | UKICU | *Bei ya sasa* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mnada Uliopita* | 1,720 | 1,720 |
| | | ***Mabadiliko (%)*** | | |

Alama (▲▼▶ ) zinaonyesha mwelekeo wa mabadiliko ya bei:
(▲) Bei imeongezeka; ( ▼ ) Bei imeshuka; (▶) Hakuna mabadiliko ya bei.

## 5.0 UHAMASISHAJI MATUMIZI NA UWEKEZAJI KATIKA BIDHAA ZA KOROSHO NCHINI

### 5.1 Jinsi ya kuandaa Maziwa ya korosho kwa matumizi ya nyumbani

Maziwa ya korosho ni mojawapo ya bidhaa itokanayo na zao la korosho na huandaliwa kupitia korosho karanga nyeupe (cashew kernel). Kwa mujibu wa tafiti mbalimbali za kiafya maziwa ya korosho yana faida nyingi za kiafya katika mwili wa binadamu ikiwemo kusaidia uimara wa mifupa, afya ya moyo, upunguzaji wa uzito n.k.  Maziwa ya korosho ndiyo bora kabisa, kwa kutoa "cream" thabiti tofauti na aina nyingine ya jamii ya karanga



### 5.2 Hatua za maandalizi

- Loweka kikombe kimoja cha korosho kwa masaa 4 au usiku kucha kwenye jokofu ili kulainisha korosho hizo kwa ajili ya kusaga;
- Chuja maji na zioshe/zisuuze kwa maji mara mbili au tatu hadi maji yatakapokua bila rangi (Clear).
- Weka korosho na vikombe vinne vya maji (ongeza ladha yoyote upendayo kama vile vanilla, chocolate, strawberry) katika mashine ya kusaga (high powered blender)
- Saga kwa spidi ya chini, kisha ongeza kasi taratibu hadi zitakapokua zimesagika na kuwa maziwa (creamy). Zoezi hili linachukua dakika 2 katika "blender" yenye nguvu kubwa au muda zaidi kwa blenda ya uwezo mdogo.
- Mimina katika chombo chako na hifadhi katika jokofu tayari kwa kutumia

### 5.3 Taarifa za Lishe na Matumizi ya maziwa ya korosho.

Maziwa ya korosho yakihifadhiwa vizuri kwenye jokofu yanaweza kudumu kwa muda wa siku 3 hadi 4 pasipo kuongeza kemikali yoyote ya kuhifadhia. Maziwa ya korosho yana kalori chache kuliko maziwa ya wanyama na mimea mingine na ni mbadala sahihi wa maziwa ya ng'ombe kwa wale wasioweza kutumia maziwa ya ngombe kwa sababu mbalimbali za kiimani au kiafya.



**Maziwa ya Korosho**

**Chanzo: Akros**

**MAWASILIANO**
**MKURUGENZI MKUU**
**BODI YA KOROSHO TANZANIA**
**S.L.P 533 TANU ROAD – MTWARA**
**Simu: +255 (23) 233 3303/233 3450**
**Barua pepe: info@cashew.go.tz**
**Tovuti: www.cashew.go.tz**